

Hakikisha una angalau simu moja inayofanya kazi nyumbani kwako



Piga simu namba 911 kama una dharura ya aina yoyote. Kama unahitaji mtafsiri, kutakuwa na muda kidogo wa ukimya kwa kungojea. Simu ikitatika, piga tena 911.



Kuwa tayari kutoa taarifa zote muhimu kama vile aina ya dharura uliyonayo, mahali ulipo, na kama silaha zimetumika.



Usipige simu namba 911 kwa tukio ambalo siyo la dharura, kwa sababu kwa kufanya hivyo unaweza kusababisha mtu anayehitaji msaada wa dharura kukosa huduma.



IDARA YA POLISI YA BOWLING GREEN

WASILIANA NASI SIMU NAMBA

DHARURA 911

KAMA SI DHARURA 270-393-4000

Shukurani maalum kwa Idara ya Zimamoto ya Bowling Green; Idara ya Huduma za Dharura ya Medical Center; na kwa Joe Imel wa Gazeti la Bowling Green Daily News kwa mchango wake wa picha.

KAMA KUNA

DHARURA

PIGA SIMU

NAMBA 911



Imechapishwa na Idara ya Polisi ya Bowling Green

Simu Namba 911 ni kwa aina YOYOTE ya dharura ...

Namba 911 ni namba ya simu kwa aina ZOTE za dharura. Kama unahitaji Polisi, zimamoto, au gari ya wagonjwa unaweza kupiga simu namba 911. Pia hajjalishi kama unaishi ndani ya mji wa Bowling Green, kwenye wilaya yako au popote pale kwenye jimbo la Kentucky. Kama una dharura piga simu namba 911. Mhudumu wa simu atakayekupokea atatuma kwako msaada unaofaa kwa dharura uliyonayo.



Usikate simu ...

Hata kama huongei Kiingereza vizuri au hujui kuongea Kiingereza kabisa wahudumu watakaopokea simu ya namba 911 wanaweza kukusaidia kwa kukuunganisha na mtafsiri wa lugha yako. **Hata kama** inaweza kuonekana kama vile simu imekatwa, USIKATE SIMU. Mara tu mhudumu atakapoweza atakuunganisha na mtafsiri bila malipo yoyote. Jaribu kutulia na msaada utatolewa.

Taarifa itakayohitajika kwa mhudumu wa namba 911...

Kitu cha kwanza mhudumu atakwambia "hapa ni 911, dharura yako ni nini?" Mhudumu atakuulizia:
Uko mahali gani?
Kitu gani kinatokea?
Kuna mtu yeyote aliyeyumia?
Kuna silaha zozote zilizotumika?



Piga simu namba 911 uwapo na dharura tu...

Kupiga simu namba 911 kwa tukio ambalo si dharura inaweza kusababisha kucheleweshwa kwa huduma kwa mtu mwenye dharura. Piga simu namba 911 kwa dharura tu, kama vile uhalifu unaoendelea, moto, au kuomba gari la wagonjwa kwa ajili ya dharura ya ugonjwa. Kwa mahitaji mengine ambayo siyo ya dharura piga simu namba 270-393-4000.

Pia, usiruhusu watoto wadogo kuchezea simu. Kuna simu nyingi zinapokelewa katika vituo vya namba 911 ambazo zinatokana na watoto wanaochezea simu. Wafundishe watoto wako matumiziyanayofaa ya kutumia mfumo wa namba 911.

